# MUHTASARI WA KIKAO CHA KUJADILI JINSI YA KUWAWEZESHA DSFA KUTUMIA MFUMO WA e-OFFICE UNAYOTUMIWA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA, KILICHOFANYIKA KUPITIA MFUMO WA eMIKUTANO TAREHE 15 JUNI, 2023

## A MAHUDHURIO

| | Jina | Ushiriki | Taasisi | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|
| A.1 | Joan Valentine | Mwenyekiti | e-GA | joan.valentine@ega.go.tz |
| A.2 | Kulwa Kapama | Mjumbe | e-GA | kulwa.kapama@ega.go.tz |
| A.3 | Gideon Mbago | Mjumbe | e-GA | gideon.mbago@ega.go.tz |
| A.4 | Donald Samweli | Mjumbe | e-GA | donald.samweli@ega.go.tz |
| A.5 | Ahmad Mtele | Katibu | e-GA | ahmad.mtele@ega.go.tz |
| A.6 | Fatma Saad | Mjumbe | e-GAZ | fatma.saad@egaz.go.tz |
| A.7 | Abdallah Juma Ali | Mjumbe | e-GAZ | abdalla.ali@egaz.go.tz |
| A.8 | Khalid Abdalla Mohamed | Mjumbe | DSFA | khalid.mohamed@dsfa.go.tz |
| A.9 | Honorat Kempanju | Mjumbe | DSFA | honorat.kempanju2@dsfa.go.tz |
| A.10 | Abdulrahman Abdulrahman | Mjumbe | ZICTIA | abdulrahman.abdulrahman@zictia.go.tz |

## B AJENDA

1. Kufungua Kikao
2. Utangulizi
3. Kujadili jisni ya kuwawezesha DSFA kutumia e-office inayotumia na Serikali ya Jamhuri ya Muungango wa Tanzania
4. Maazimio
5. Kufunga Kikao

## C AJENDA 1- KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao **saa 09:30 alasiri** na kuwakaribisha wajumbe wote kwa ajili ya utambulisho.

**D AJENDA 2- UTANGULIZI**

Mwenyekiti alieleza kuwa **Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA)** ilipokea barua kutoka **Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)** ikiomba kufanya kikao cha pamoja kujadili juu ya upatikanaji wa huduma ya e-office katika Ofisi yao.

**E AJENDA 3- KUJADILI JINSI YA KUWAWAWEZESHA DSFA KUTUMIA E-OFFICE INAYOTUMIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**

Kikao kilijadili maombi hayo kwa kupokea maoni mbali mbali kutoka kwa wajumbe wa Taasisi shiriki ambazo ni DSFA,e-GA, e-GAZ na ZICTIA kama ifuatavyo.

**3.1 Ilielezwa** kuwa DSFA ni Taasisi ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo makao makuu yake yanapatikana Zanzibar. Hivyo kutokana na asili hiyo ya taasisi, DSFA inaomba kutumia mfumo wa e-office unaotumika na taasisi zilizopo Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo DSFA iliomba kuwezeshwa ili waweze kutumia huduma hii.

**3.2 Ilielezwa** kuwa jinsi ya kufikia mfumo wa e-office ni kupitia mtandao wa Serikali (GovNet), hii ni kama ilivyoainishwa kwenye “ Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa, Data na Mifumo ya Tehama Serikalini, Sura ya 3, Shemu 3.1.9.au kupitia huduma ya VPLS kwa taasisi zilizo mbali na PoP za GovNet ambapo taasisi husika itaunganishwa na mtandao wa mtoa huduma kwa njia ya layer 2 ili kuweza kupata huduma ya GovNet. Hivyo DSFA inaweza kutumia mfumo wa e-office kupitia njia ya VPLS kama ilivyo kwa taasisi nyingine zilizo mbali na GovNet.

**3.3 Ilielezwa** kuwa, kwa kuwa mtandao wa GovNet haujafika Zanzibar, basi VPLS ndio njia muafaka itakayofaa kwa kuwezesha DSFA kutumia e-office .

**3.4 Mjumbe aliuliza** kama kuna uwezekano wa taasisi moja kutumia instance mbili za e-office mfano e-office inayotumika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile inayotumika na Taasisi zilizopo kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**3.5 Ilielezwa** kuwa taasisi moja haiwezi kutumia instance mbili za e-offie. Ila kunajitihada zitafanyika hapo baadae ili kuwezesha instance mbili za e-office ziweze kuwasiliana kwa kuweza kutuma barua kutoka taasisi moja kwenda nyingine ndani ya mfumo kama ilivyo kwa taasisi zilizotumia cloud e-office.

**3.6 Mwenyekiti aliuliza** kuwa DSFA walipewa orodha ya vifaa vinavyotakiwa kununuliwa vikiwemo router na firewall je vifaa hivyo vimeshanunuliwa?.

**3.7 Mjumbe alijibu** kuwa vifaa hivyo bado havijanunuliwa ila wanafaata taratibu za manunuzi ili waweze kununa vifaa hvyo.

**3.8 Mjumbe alishauri** kuwa DSFA wanunue hivyo vifaa ili kuendelea na hatua ya kuwaunganisha DSFA kapitia VPLS.

**E AJENDA 4- MAAZIMIO**

**4.1** Kikao kilifikia maazimio kuwa DSFA watapata eoffice kama ilivyoombwa kwenye barua.

**4.2** DSFA wataunganishwa na e-office kupitia VPLS, hivyo DSFA inatakiwa wanunue vifaa ambavyo viliorodheshwa kwenye barua ya awali kwa kufuata taratibu za manunuzi kisha wawasiliane na e-GA ili kuendelea na zoezi la kuwaunganisha na e-office.

**4.3** Iliazimiwa pia, ZICTIA na e-GAZ watatoa guidance kwa DSFA kwenye ununuzi wa vifaa na usaidizi pale utakapokuwa unahitajika.

**4.4** Mwisho iliazimiwa kuwa uelekeo ni kuwa hapo baadae hizi instance mbili za e-office ambazo ziweze kuwasiliana.

**F AJENDA 5- KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alihairisha kikao mnamo **saa 11:02 jioni**. Aliwashukuru wajumbe wote kwa kushiriki katika kikao.

| | |
|---|---|
|  Digitally Signed By Joan Valentine Tue Jun 27 18:59:39 EAT 2023 ........................ Joan Valentine **Ag.MCA** |  Digitally Signed By Ahmad Mtele Tue Jun 27 19:21:50 EAT 2023 ........................ Ahmad Mtele **ICTO** |
| Joan Valentine | Ahmad Mtele |
| **Mwenyekiti - e-GA** | **Katibu - e-GA** |